JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA**

*Unapojibu tafadhali taja:*
**Kumb. Na. DEO/IRA/E10/51VOL.4/64** **03 June 2025**

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

## MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA ANAKARIBISHA MAOMBI YA KAZI KWA WANANCHI WOTE KWA MWENYE SIFA YA KUWA MLEZI (MATRON) WA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM SHULE YA MSINGI KIZEGA

Kwa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma na marekebisho yake **Na. 8 ya mwaka 2014**, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba anatangaza nafasi ya kazi kwa wenye sifa zifuatayo:

### I. SIFA YA MWOMBAJI:

a) Awe Mtanzania
b) Awe jinsia ya kike
c) Awe mwenye moyo wa huruma, upendo na mwenye wito wa kukaa na watoto wenye mahitaji Maalum
d) Awe tayari kukaa (kuishi) bweni kwa ajili ya kusimamia wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa ukaribu
e) Awe na uzoefu usiopungua mwaka mmoja katika nafasi husika
f) Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai
g) Awe mwaminifu, nidhamu na bidii ya kazi
h) Awe na umri kuanzia miaka **25** hadi miaka **45**
i) Awe mwenye akili timamu.

### II. KAZI NA MAJUKUMU

- Kusimamia usafi wa ndani ya Bweni kama kutandika vitanda, kudeki na usafi wa Wanafunzi wa bweni kwa ujumla.
- Kuwa msimamizi wa karibu wa Wanafunzi wenye mahitaji Maalum.
- Kuhakikisha kuwa kila aliyeko bwenini ni mwanafunzi halali wa bweni.
- Kuhakikisha kuwa Wanafunzi wa bweni wanafuata Sheria za Shule.

- Kuwapokea Wanafunzi kwa utaratatibu uliyowekwa na kukagua vifaa vyao mara wanaporipoti Shuleni.
- Kushirikiana na mwalimu wa zamu kwenye ugawaji wa chakula cha mchana na joini kwa wanafunzi wa bweni.
- Kuitisha majina kila asubuhi waondokapo darasani na baada ya vipindi (Kujua idadi ya Wanafunzi waliopo bweni).
- Kuhakikisha kuwa hakuna mwanafunzi mwenye kifaa hatarishi bwenini.
- Kuripoti matatizo ya Wanafunzi wa bweni kwa Mwalimu Mkuu.
- Kufanya kazi yoyote utakayoagizwa na Mkuu wako muda wa kuwa haipingani na maadili ya kazi.
- Kuhakikisha kuwa Wazazi wanaotembelea Watoto wao wanakuwa sehemu iliyotengwa na siyo bwenini.
- Utawajibika kwa Mkuu wa Shule.

## III. MAMBO YA KUZINGATIA

- Barua ya maombi iambatishwe na nakala za Vyeti vya taaluma kama ipo na Cheti cha kuzaliwa.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **30 June 2025.**
- Watakao kuwa wamekidhi vigezo vya kuitwa kwenye usahili watajulishwa.
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta tu, kwa anwani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Iramba,**
**S.L.P 155,**
**Kiomboi - IRAMBA.**

Tangazo hili limetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya.

Segu

Magreth C. Segu
**Kny:MKURUGENZI MTENDAJI**
**03 June 2025**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA IRAMBA